# MKATABA WA MAUZO YA KIWANJA CHENYE HATI

## KATI YA

## BADER MAREI NAHDI

## NA

## MUSTAFA AHMED MOHAMED

### MALI INAYOUZWA:-

TITLE NAMBA 29594, PLOT NAMBA 27/7 KILICHOPO ENEO LA MATEVES, KATIKA WILAYA YA ARUMERU, MKOANI ARUSHA

**MKATABA HUU UMEANDALIWA NA:-**

**Gwakisa Kakusulo Sambo, Wakili**
Patriotic Legal Consultants
& Co. Advocates
Makongoro Road
2nd Floor, CCM Building
Room No. 6, 16 & 17
P. O. Box 16081
ARUSHA.
Simu: 0752 129603

gwakisa2011@gmail.com

Saini Ya Muuzaji.................................... Saini Ya Mnunuzi....................................

Scanned with CamScanner

# MKATABA WA MAUZO YA KIWANJA CHENYE HATI

**MKATABA** huu umefanyika leo siku ya tarahe **02** mwezi **10** mwaka **2019 KATI** ya **BADER MAREI NAHDI** wa S. L. P 10305, **ARUSHA** kwa upande mmoja (ambaye katika mkataba huu ataitwa **"MUUZAJI"**),

**NA**

**MUSTAFA AHMED MOHAMED** wa S. L. P 398, **ARUSHA** kwa upande mwingine (ambao katika mkataba huu ataitwa **"MNUNUZI"**).

**WAKATI AMBAPO;-**

Muuzaji ni mmiliki halali wa kiwanja chenye **Title** Namba **29594, Plot Namba 27/7** kilichopo eneo la **Mateves**, katika Wilaya ya **Arumeru**, Mkoani Arusha chenye ukubwa wa meta za mraba **3244.**

**NA WAKATI AMBAPO;-**

Muuzaji ana nia ya kuuza na kuhawilisha umilikaji wa kiwanja **Title** Namba **29594, Plot Namba 27/7** kilichopo eneo la **Mateves**, katika Wilaya ya **Arumeru**, Mkoani Arusha chenye ukubwa wa meta za mraba **3244** pamoja na mastawisho mengine yaliyozunguka kiwanja hicho na mnunuzi pia anayo nia ya kununua kiwanja hicho pamoja na Mastawisho yake yaliyopo kwa makubaliano na masharti yafuatayo;-

## SASA INAKUBALIKA KAMA IFUATAVYO;-

**UFAFANUZI;-**

Mkataba huu ni wa Mauzo ya kiwanja/plot na unaainisha vitu vifuatavyo;-

***"Mkataba"*** inamaanisha Mkataba huu wa Mauzo unaopelekea kwenye uhawilishaji/ mauzo ya kiwanja **Title** Namba **29594, Plot Namba 27/7** kilichopo eneo la **Mateves**, katika Wilaya ya Arumeru, Mkoani Arusha chenye ukubwa wa meta za mraba **3244**

***"Pande Husika"*** Inamaanisha watia sahihi katika Mkataba huu.

Saini Ya Muuzaji.................................................. Saini Ya Mnunuzi...................................................

Scanned with CamScanner

*"Fedha ya Mauzo"* Inamaanisha kiasi cha shilingi za kitanzania shilingi **MILIONI THEMANINI** tu (**Tshs. 80,000,000/=**), Ambazo zitalipwa zote kwa mkupuo.

*"Shs"* Inamaanisha fedha halali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

1. **KWAMBA,** muuzaji anamuuzia mnunuzi na mnunuzi ananunua eneo linalofahamika kiwanja chenye **Title** Namba **29594, Plot Namba 27/7** kilichopo eneo la **Mateves**, katika Wilaya ya Arumeru, Mkoani Arusha chenye ukubwa wa meta za mraba **3244** kwa malipo ya shilingi milioni themanini tu **(TShs.80,000,000/=)** tu.

2. **KWAMBA,** Mnunuzi atamlipa Muuzaji fedha ya mauzo kwa awamu moja mara baada ya kusaini mkaba huu.

3. **KWAMBA,** mara baada ya kusaini mkataba huu mnunuzi atafanya utaratibu wa kuhamisha **(Transfer)** umiliki wa kiwanja hicho kwenda kwa jina lake. Pia muuzaji atatakiwa akabidhi hati zote zinazohusu kiwanja hicho na Mastawisho yake kwa mnunuzi mara baada ya Malipo yote kufanyika yanayohusiana na ununuzi wa eneo tajwa.

4. **KWAMBA,** muuzaji anathibitisha kuwa;-

   **4.1 Kwamba,** kiwanja hicho, haijawekwa rehani kwa mtu yeyote au shirika au benki yoyote iwayo.

   **4.2 Kwamba,** kwa kuingia kwenye Mkataba huu muuzaji hatakuwa amevunja Mkataba mwingine wowote, pia hatakuwa amevunja amri yoyote ya Mahakama au Mamlaka yeyote iwayo.

5. **KWAMBA,** Mnunuzi anathibitisha pia kuwa;-

   5.1 Anafahamu vema kiwanja hicho pamoja na Mastawisho yaliyopo.

   5.2 Kwamba ameikagua na ameridhika nayo pamoja na mastawisho yake.

   5.3 Kwamba hatakuwa na madai yoyote yatokanayo na hali **(condition)** ya mazingira hayo.

Saini Ya Muuzaji.................................... Saini Ya Mnunuzi....................................

Scanned with CamScanner

6. **KWAMBA,** muuzaji na mnunuzi wanakubaliana kwamba kukamilika kwa Mkataba huu kutategemea vitu vifuatavyo;-

6.1.1 Utakapofanyika usajili wa mnunuzi kama mmiliki halali wa kiwanja husika.

6.1.2 Mkataba huu wa mauzo unajumuisha makubaliano yote ya pande mbili kuhusu mambo yote yaliyotajwa katika Mkataba huu. Chochote kisichokuwepo kwenye Mkataba huu hakitakuwa na nguvu ya kisheria kwa pande zote mbili.

6.1.3 Mkataba mwingine wowote unaojaribu kutofautisha kuongoza, kuondoa au kufuta chochote kilichopo kwenye Mkataba huu hautakuwa na nguvu ya kisheria labda uwe umewekwa katika Maandishi na kusainiwa na pande zote mbili.

7. **KWAMBA,** endapo upande wowote utavunja sharti lolote la Mkataba huu basi upande utakaokuwa umedhurika utakuwa na haki ya kufungua Shauri la madai au jinai kwenye Mahakama inayostahili kupata haki yake.

**MKATABA HUU** umefanyika leo hii tarehe **02** mwezi **Oktoba**, 2019 na kwa kuthibitisha hayo hapo juu pande zote mbili zimeridhika zimekubaliana kuweka saini zao wakiwa na akili timamu bila kushurutishwa/kushawishiwa/kulazimishwa na Mtu yeyote yule Mbele ya Wakili na Mashahidi wafuatao:-

**MKATABA HUU hapa Arusha** umesainiwa na **BADER MAREI NAHDI** ambaye ninamfahamu binafsi leo tarehe **02** mwezi **Oktoba, 2019** } [signature] **MUUZAJI**

**Mbele ya Wakili**

Jina Kamili: SAID AMRI

Saini: [signature]

Anuani: S.L.P 16081, ARUSHA

Cheo : Wakili/Kamishina wa Viapo

SAID AMRI ADVOCATE NOTARY PUBLIC & COMMISSIONER FOR OATHS P.O.BOX 16081, ARUSHA

Saini Ya Muuzaji........[signature]........ Saini Ya Mnunuzi........[signature]........

Scanned with CamScanner

**MKATABA HUU hapa Arusha** umesainiwa na **MUSTAFA AHMED MOHAMED** amabae ninamfahamu binafsi leo tarehe **02** mwezi **Oktoba, 2019**

**MNUNUZI**

**Mbele ya wakili**

Jina Kamili: SAID AMRI

Saini:

Anuani: S.L.P 16081, ARUSHA

Cheo : Wakili/Kamishina wa Viapo

SAID AMRI ADVOCATE NOTARY PUBLIC & COMMISSIONER FOR OATHS P.O.BOX 16081, ARUSHA

**Umeandaliwa na:**

**Gwakisa K. Sambo, (Wakili)**
Patriotic Legal Consultants
& Co. Advocates, CCM(R) Building, 2nd Floor,
Room No.13, 16 &17
P.O Box 16081,
Arusha.
**Mobile Number;** 0752129603/0714129603
**Email:** gwakisa2011@gmail.com

Saini Ya Muuzaji........................................ Saini Ya Mnunuzi........................................

Scanned with CamScanner